

Karibuni kwa Mafunzo na Elimu ya Mbali ya OTEN. OTEN ni TAFE ya NSW ambayo ina utaalamu wa kusomesha kwa umbali yani “distance learning”. Unaweza kujiandikisha kwa masomo haya wakati wowote.

Ukiwa unataka kuongeza ustadi wa kazi yani “employment skills”, ama kuanza kazi ya kiwango ya juu zaidi ya ile unafanya ama ungetaka kusoma kwa sababu unapenda kuongeza ufahamu **wa hiyo** kosi, OTEN ndio chaguo lako.

OTEN inasomesha zaidi ya kosi 250. Nyingi za hizi kosi zimetambuliwa na Australian Qualifications Framework. Masomo haya yanasomeshwa kama masomo ya umbali kwa uhusiano, yani “correspondence” na kwa compyuta.

Unaweza kuchagua kosi ile inafaa wewe ata ikiwa lugha yako ya kizungu haijatimia, ama uko na ulemavu, ama unaishi mbali sana. Ikiwa huna hakika juu ya ile kosi anataka kufanya unaweza **kuongea** na mwalimu wa OTEN kwa usaidizi.

Uko na masomo au ujuzi kutoka ng’ambo? Unajua hii masomo au ujuzi inaweza kufahamiwa wakati unaongeza masomo ama wakati unatafuta kazi huku Australia. Wasaidizi wa wanafunzi wa taaluma mbalimbali, wanaojulikana kwa kizungu kama Multicultural Education Support Unit wanaweza kukusaidia ili hii masomo itambulike.

Kwa maelezo zaidi juu ya OTEN na kosi zile tunasomesha pigia wajulisha kosi wa OTEN kwa nambari 02 9715 8333 au 1300 362 346

Ikiwa uko na shida ya kuongea Kiingereza na unahitaji usaidizi kutafsiri tunaweza tukusaidia na mtafsiri.